

Tanzania, Mawe, Ajira kwa Watoto

Kuna ushahidi kwamba watoto walio na umri wa chini ya miaka 18 wanahusika katika uzalishaji wa mawe nchini Tanzania. Kutokana na uchambuzi wa Uchunguzi Jumuishi wa Nguvu Kazi Tanzania wa mwaka 2020/21, inakadiriwa kuwa watoto 10,634 walio chini ya umri wa kufanya kazi huchimba mawe nchini kote, hususani katika mikoa ya Dodoma na Geita. Watoto wanaofanya kazi kwenye maeneo ya machimbo hufanya kazi kama vile kusaga na kuvunja miamba ili kutengeneza kokoto na kusafirisha mawe na changarawe. Kuna matatizo mengi ya kiafya na kiusalama yanayohusiana na kufanya kazi kwenye maeneo ya machimbo, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwenye miinuko hatari, kubeba mizigo mizito, na kutumia zana na vifaa hatari (ikiwa ni pamoja na vilipuzi), kwa ujumla bila upatikanaji wa vifaa vya kinga. Serikali ya Tanzania inapaswa kupongezwa kwa sababu ya kuendesha na kuchapisha data za uchunguzi zinazosaidia kubuni na kutekeleza sera na programu madhubuti za kukabiliana na ajira kwa watoto.